# Karatasi ya taarifa kuhusu uchunguzi wa mlango wa kizazi

Swahili

## Kipimo cha uchunguzi wa mlango wa kizazi ni nini?

Kipimo cha uchunguzi wa mlango wa kizazi huchunguza afya ya kizazi chako. Mlango wa kizazi ni uwazi wa kuelekea kwenye tumbo lako la uzazi kutokea ukeni kwako. Kipimo cha HPV cha Mlango wa Kizazi mojawapo ya njia bora za kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi.

Sio kipimo cha saratani. Ni kipimo ambacho kinaweza kusaidia kuzuia saratani kukua.

Ni mojawapo ya njia bora za kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi kwa hiyo usichelewe kufanyiwa uchunguzi wa mlango wa kizazi kila muda unapofika.

## Kipimo cha HPV cha Mlango wa Kizazi ni nini?

Hii ni njia mpya ya uchunguzi kwenye mlango wa kizazi. Kinaitwa kipimo cha HPV cha Mlango wa Kizazi na kilianzishwa nchini Ayalandi mnamo mwaka 2020. Aina hii ya uchunguzi wa kizazi tayari imeanzishwa nchini Australia, Uholanzi, Uingereza na Wales. Sampuli yako ya uchunguzi wa mlango wa kizazi huchunguzwa kwanza kwa virusi vya papilloma ya binadamu (HPV) – virusi ambavyo vinaweza kusababisha saratani ya mlango wa kizazi.

Kama HPV vitapatikana, sampuli hiyo hiyo itapimwa ili kama una mabadiliko yoyote yasiyo ya kawaida (kabla ya saratani) ya seli katika mlango wa kizazi chako.

Njia hii ya uchunguzi:

- ni njia bora ya uchunguzi wa mlango wa kizazi
- huzuia saratani zaidi
- inamaanisha baadhi ya watu watakuwa na vipimo vichache

Kama umeshawahi kufanya kipimo cha pap, kufanya kipimo cha mlango wa kizazi kutakufanya ujisikie vile vile.

## Kipimo cha HPV cha mlango wa kizazi hufanywaje?

Kwa kawaida kipimo huchukua takriban dakika 5.

1. Utaombwa uvue nguo kuanzia kiunoni na kushuka na ulale kwenye kochi.
2. Unaweza kulala upande au kulalia mgongo, vyovyote utakavyojisikia.
3. Daktari au muuguzi ataweka kwa taratibu chombo kinachoitwa speculum kwenye uke wako. Hii inashikilia kuta za uke kuwa wazi, ili waweze kuuona mlango wa kizazi chako.
4. Brashi ndogo, laini itatumika kukusanya kwa taratibu sampuli ya seli kutoka kwenye mlango wa kizazi.

Watu wengine huona zoezi hili kuwa lenye kro au la kuaibisha, lakini kwa wengi wao, halina maumivu. Kama unaona kuwa kipimo kinakuumiza, mwambie daktari au muuguzi kwani anaweza kupunguza maumivu kwako.

## Uchunguzi wa mlango wa kizazi una faida gani?

Uchunguzi wa HPV wa mara kwa mara kwenye mlango wa kizazi:

- huokoa maisha
- unaweza kupata HPV kabla ya haijasababisha seli zisizo za kawaida kwenye shingo ya kizazi
- unaweza kupata mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli kabla ya dalili kutokea
- unaweza kupata mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli katika kipindi ambacho ni rahisi kutibu

Kugundua HPV na seli zisizo za kawaida mapema ni njia bora ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kukua.

Ndio maana ni muhimu kufanya uchunguzi wa mara kwa mara.

## Je, kuna mapungufu gani ya uchunguzi wa mlango wa kizazi?

Mapungufu makuu ya uchunguzi wa mlango wa kizazi ni:

- uchunguzi wa mlango wa kizazi hautazuia visa vyote vya saratani ya mlango wa kizazi
- watu wengine bado watapata saratani ya mlango wa kizazi licha ya uchunguzi wa mara kwa mara
- baadhi ya mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli yanaweza yasionekane
- uchunguzi hautagundua kila mabadiliko ya seli yasiyo ya kawaida
- wakati mwingine matokeo ya vipimo huwa si sahihi

## Sampuli yangu hufanyiwa nini?

Sampuli yako itaenda kwenye maabara iliyohakikishiwa ubora (maabara). Katika maabara sampuli yako itapimwa ili kuona kama una maambukizi ya HPV. Kama una maambukizi amilifu ya HPV, wataalamu wawili watachunguza sampuli yako kuona kama kuna mabadiliko ya seli. Ikiwa watagundua mabadiliko yoyote, utahitaji kipimo cha ufuatiliaji linaloitwa kolposkopi. Kolposkopi ni uchunguzi wa kina zaidi kwenye kizazi chako.

## Kwa nini mabadiliko mengine yasiyo ya kawaida katika seli hayaonekani?

Kwanza, sampuli yako itachunguzwa kama ina HPV. Kama HPV vitapatikana, pia itakaguliwa kwa seli zisizo za kawaida.

Lakini sio kila mtu anayepata saratani ya mlango wa kizazi atakutwa na HPV wakati wa uchunguzi.

Kipimo hasi cha HPV – ambapo HPV havikuonekana – pia hakimaanishi kuwa hutapata maambukizi katika siku zijazo.

Mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli wakati mwingine hayataonekana kwa sababu:

- wakati mwingine seli zisizo za kawaida zinaweza kuonekana sawa na seli za kawaida
- kunaweza kuwa na seli chache sana zisizo za kawaida kwenye sampuli
- mtu anayechunguza sampuli yako anaweza kukosa kuziona seli zisizo za kawaida (hii hutokea wakati mwingine, bila kujali ana uzoefu gani)

Hakuna kipimo katika programu yoyote ya uchunguzi kitakachopata kila mtu ambaye ana seli za mlango wa kizazi zisizo za kawaida.

# Information sheet on cervical screening



Saratani ya mlango wa kizazi huchukua miaka mingi kukua. Mara nyingi, inachukua miaka 10 hadi 15 kwa seli kubadilika kutoka kuwa kawaida hadi isiyo ya kawaida hadi saratani.

Ndio maana kila wakati unapaswa kwenda kwenye uchunguzi wa mlango wa kizazi kila muda unapowadia.

## Nitajuaje kuhusu matokeo ya kipimo nilichofanya?

Matokeo yako yatatumwa kwako kwa njia ya posta, kwa kawaida ndani ya wiki 4 za kipimo. Pia kitatumwa kwa daktari wako au kliniki.

## Matokeo yangu yanamaanisha nini?

Kuna matokeo manne yanayoweza kupatikana.

**1. HPV havijapatikana**

Matokeo yako yanaonyesha kuwa huna maambukizi ya HPV kwa wakati huu. Utafanyiwa kipimo kijacho cha uchunguzi wa kizazi baada ya miaka 3 au 5 kulingana na umri wako.

**2. HPV vimepatikana na hakuna mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli yaliyopatikana**

Matokeo yako yanaonyesha kuwa una maambukizi ya HPV lakini hakuna mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli yalionekana. Unapaswa kufanya kipimo kingine ndani ya miezi 12. Hii itatoa muda kwa mwili wako ili kuondokana na maambukizi ya HPV.

**3. HPV na mabadiliko ya seli yasiyo ya kawaida yamegundulika**

Matokeo yako yanaonyesha una maambukizi ya HPV na mabadiliko yasiyo ya kawaida ya seli kwenye mlango wa kizazi chako. Unahitaji kipimo cha kufuatilia kinachoitwa kolposkopi - uchunguzi wa kina zaidi wa mlango wa kizazi chako. Ni sawa na kufanyiwa uchunguzi wa mlango wa kizazi.

**4. Sampuli isiyotosha**

Hii inamaanisha kuwa maabara haikuweza kuchakata sampuli yako ya uchunguzi. Utaombwa kurudia uchunguzi wa mlango wa kizazi chako ndani ya miezi mitatu.

## Kutoa idhini yako

Kila unapofanya uchunguzi wa mlango wa kizazi tutakuomba utoe idhini yako kwa kusaini fomu ya uchunguzi wa mlango wa kizazi kabla ya kipimo. Kama huwezi kutia saini kwenye fomu, utaombwa kutoa idhini yako kwa kutamka au kwa kuweka alama kwenye fomu mbele ya daktari au muuguzi.

Hii ni kuthibitisha kuwa:

- umeambiwa kuhusu uchunguzi wa mlango wa kizazi na faida na hasara zake
- unaelewa taarifa hii
- umeangalia kwamba jina lako, anwani na maelezo mengine ni sahihi (hii inatusaidia kuthibitisha kwamba tuna anwani yako ya sasa ya kuwasiliana nawe)
- umeturuhusu kupokea, kushikilia na kubadilishana taarifa zako binafsi na historia ya uchunguzi na wale wanaoendesha programu ya uchunguzi wa HPV ya mlango wa kizazi

**Kumbuka:** Ni wewe tu ndio unayeweza kutoa idhini yako ya kuwa sehemu ya programu yetu. Lazima utoe idhini kabla ya kufanya kipimo. Unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote kwa kuwasiliana nasi kwenye Freephone **1800 45 45 55** au kutuma barua pepe **info@cervicalcheck.ie**

Hii inamaanisha kuwa hatutawasiliana nawe kuhusu programu ya uchunguzi wa mlango wa kizazi katika siku zijazo.

## Tunatumiaje taarifa zako binafsi?

Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi huchukua na kuhifadhi kwa usalama taarifa zako binafsi (jina, anwani, namba ya simu, tarehe ya kuzaliwa, PPSN, jina la ukoo wakati wa kuzaliwa na jina la mama la usichana) na historia ya uchunguzi wa mlango wa kizazi. Historia yako ya uchunguzi wa mlango wa kizazi inahusiana na ushiriki wako katika Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi.

Inaweza kujumuisha matokeo ya uchunguzi wa HPV ya mlango wa kizazi, mahudhurio ya kolposkopi, matibabu na matokeo ya biopsy (sampuli ya vipimo).

Tutatumia taarifa zako kuwasiliana na wewe wakati kipimo chako kijacho kitakapokuwa tayariau matokeo yako yatakapopatikana. Pia tunabadilishana taarifa zako na huduma nyingine za afya zinazofanya programu hii. Hii ni pamoja na daktari au muuguzi anayefanya kipimo chako cha uchunguzi, maabara, kliniki za kolposkopi na Masjala ya Saratani ya Taifa Ayalandi. Hii ni ili kudumisha na kuboresha ubora wa huduma.

Tunaweza kutumia sampuli ya kipimo chako katika mafunzo, katika tathmini na ukaguzi na kuangalia ubora na ufanisi wa programu. Tunaweza pia kutumia taarifa zako kukualika ushiriki katika utafiti.

Ni hiari yako kushiriki katika uchunguzi au la. Kamwe hatutatumia jina lako katika ripoti zozote, wakati wa kufundisha au katika tathmini. Tutahifadhi kwa usalama taarifa zako binafsi na kwa faragha kulingana na sheria za sasa za ulinzi wa data.

Utakuwa na ufikiaji kamili na wa wazi wa taarifa zako binafsi zinazoshikiliwa na Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi unapoomba. Ni muhimu ujulishe Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi kama taarifa zako zitabadilika. Ili kujua jinsi ya kufikia taarifa zako, angalia **hse.ie/gdpr/data-requests/**

Kwa taarifa zaidi angalia Ilani ya Faragha ya HSE – Wagonjwa na Watumiaji wa Huduma kwenye **hse.ie/gdpr/**

## Kuwasiliana nawe

Tutawasiliana nawe kwa uwazi, uaminifu na kwa wakati kama:

- kuna tatizo katika huduma unayopatiwa
- unapata madhara kutokana na huduma unayopatiwa
- tunadhani kuwa madhara yanaweza kuwa yametokea

Hii inamaanisha kuwa tutakujulisha ukweli kwa ukamilifu na maelezo kuhusu ushiriki wako katika programu ya uchunguzi wa mlango wa kizazi.

Tutakapopata matokeo yako, tutayatuma kwako yakiwa na taarifa zaidi kuhusu maana yake. Unaweza pia kupata taarifa zaidi kwenye **hse.ie/cervicalcheck**

# Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi
## Fomu

CervicalCheck
AN CLÁR NÁISIÚNTA SCAGTHÁSTÁLA CEIRBHEACS
THE NATIONAL CERVICAL SCREENING PROGRAMME

Swahili

**Fomu ambazo hazijakamilika kujazwa zinaweza kurudishwa.**
Tafadhali thibitisha kwa mteja kwamba maelezo yote kwenye fomu ni sahihi.
Mara baada ya kuthibitishwa tafadhali ondoa lebo ya namba ya kichupa kutoka kwenye kichupa cha sampuli na uambatanishe kwenye fomu.

Namba ya Kichupa:

Sample

### Maelezo ya Mteja

Namba ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (Namba / Barua/ Herufi)

Kitambulisho cha CSP

Namba ya Hospitali (ikiwa inatumika)

Tarehe ya Kuzaliwa (Siku / Mwezi / Mwaka)

Kitambulisho cha Afya ya Mtu Binafsi (IHI)

Jina la ukoo Tumia HERUFI KUBWA unapojaza taarifa zako

Jina la Kwanza

Jina la Kati

Jina la Ukoo la Kuzaliwa

Jina la Usichana la Mama

Anwani ya Posta kwa Mawasiliano

Msimbo wa Eir:

Namba ya Simu ya Mawasiliano

Tafadhali hakikisha kwamba maelezo yako yaliyo hapo juu ni sahihi

**Ninaelewa taarifa niliyopewa. Ninakubali kushiriki katika Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi**

Saini ya Mteja: ____________________

Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi haipokei idhini ya mtu mwingine.

### Daktari / Muuguzi

Jina la Daktari / Muuguzi:

Hospitali / Kliniki:

Anwani:

Kitambulisho cha Daktari / Muuguzi: (MCRN au Namba ya NMBI)

Namba ya Simu

Kitambulisho cha Daktari Anayewajihusika au Kitambulisho cha Kliniki (MCRN)

Tarehe ya Kipimo (Siku / Mwezi / Mwaka) LMP (Siku / Mwezi / Mwaka)

**Maelezo muhimu ya Kliniki** (tafadhali weka alama kama inavyofaa)

OCP/Homoni/HRT ☐ IUCD ☐ Baada ya Ukomo wa Hedhi ☐
Amechanjwa HPV ☐ Kipimo cha Pap baada ya Kolposkopi ☐
Jumla ndogo / Jumla ya Utoaji KIzazi ☐ Kabla/Baada ya Kupandikiza ☐
Dialisisi ☐ DES ☐ CD4i ☐ Kuvuja damu baada ya ngono ☐
Kutokwa na damu baada ya ukomo wa hedhi ☐

Eneo la Sampuli: Mlango wa kizazi ☐ Kuba (jumla ya utoaji kizazi) ☐

Pale ambapo mlango wa kizazi upo, mfanya kipimo cha papp lazima auone mlango wa kizazi wote na kuupima kwa usahihi kwa mzunguko wa 5 x 360° wa sampuli. Uwasilishaji wa sampuli ni uthibitisho kwamba hili limefanywa.

Historia ya Uchunguzi

| Jina la Maabara | Tarehe ya Kipimo | Matokeo ya Kipimo cha Seli | Matokeo ya HPV |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Historia ya Matibabu

| Jina la Kliniki | Tarehe | Utaratibu | Matokeo |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

### KWA MATUMIZI YA MAABARA TU

Tarehe Ilipopokelewa katika Maabara (Siku / Mwezi / Mwaka)

Namba ya Sampuli:

Msimbo pau

Seli za TZ Ndiyo ☐ Hapana ☐

Ripoti ya Mwisho

Usimamizi Unapendekezwa

1° 2°

Njia

Tarehe Iliporipotiwa (Siku / Mwezi / Mwaka)

Saini (Siku / Mwezi / Mwaka)

CS/PUB/CC-68 Rev 1